BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kuendelea kutukarimu neema ya uhai na afya njema sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa hali ya amani na utulivu. Aidha, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wawili wa Baraza kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu yenu ya kutuongoza katika Baraza wakati tukiendelea kutekeleza wajibu wetu wa kikatiba wa kuidhinisha bajeti kwa niaba ya wananchi wetu ambao tunawawakilisha. Kwa ruhusa yako, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lakoTukufu Maoni ya Kamati ya Uchumi juu ya mchakato mzima wa makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa moyo wa dhati kabisa napenda kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake mahiri ambao kwa muda mfupi umewajengea imani na matumaini makubwa wananchi wa Zanzibar katika harakati za kujikomboa na umasikini, kujenga jamii yenye umoja na mshikamano pamoja na kuiletea maendeleo na ustawi

nchi yetu ya Zanzibar. Aidha, niwapongeze pia wasaidizi wake wa karibu Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdullah kwa namna wanavyojitolea kwa moyo wao wote katika kumsaidia Mhe. Rais katika kufanikisha malengo ya nchi yetu tuliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inatoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa ushirikiano anaotupatia katika utekelezaji wa majukumu yetu kwa Wizara yake. Kamati pia inatoa pongezi kwa watendaji wa Wizara haswa kwa Katibu Mkuu wa Wizara hii, Wakurugenzi na watendaji wote wa wizara hiyo kwa ushirikiano wao wanaompa Waziri wao pamoja na Kamati unaopelekea majukumu ya Kamati kwa Wizara hii kutekelezeka kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda niwapongeze Waheshimiwa Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu kwa juhudi wanazozichukua za kuwawakilisha wananchi wao, juhudi zao zimewawezesha Wananchi kujenga imani kubwa kwa Baraza Lako. Nasi tunawaahidi kwamba tutaendelea kuwatumikia kwa dhati kama walivyotuamini kutuchagua na kutuleta katika chombo hiki kwa lengo la kutetea maslahi yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uchumi kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisishia kazi yangu ya kuongoza vikao kuwa nyepesi zaidi, kwa hakika ni Wajumbe mahiri, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoziidhinisha kwa Wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Wajumbe wa Kamati ya Uchumi walifanya kazi kubwa ya kuipitia kwa kina Bajeti ya Fungu L02 (Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi) na kufanya marekebisho madogo madogo. Naomba sasa niwatambue kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda - M/Mwenyekiti

3. Mhe. Rukia Omar Ramadhan - Mjumbe

4. Mhe. Hassan Hamad - Mjumbe

5. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe

6. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe

Sambamba na hilo, Kamati yangu inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Panya Ali Abdalla kwa mashirikiano anayoipatia Kamati licha ya kuwa kwenye udhuru uliopelekea kutofika kwenye shughuli za Kamati, baada ya kuondokewa na mwenza wake, lakini amekua akichangia na kuchambua bajeti zote zilizowasilishwa mbele ya Kamati yetu, ikiwa ni pamoja na hii ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. michango yake amekua akiwasilisha kwa njia ya maandishi na imekuwa na tija kubwa kwa kamati yetu na wizara kwa ujumla.

Aidha, Kamati yetu inafanyakazi kwa karibu sana na makatibu wawili (2) ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia kutekeleza majukumu yetu, kwa heshima naomba nao niwatambue:

1. Ndugu Nouman Thabit Nouman - Katibu

2. Ndugu Asma Ali Kassim - Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imefanya kazi ya kuchambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, siku ya tarehe 03/05/2023, kwa kuzingatia matakwa ya Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa Bajeti inayozingatia program (PBB), Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Fungu Kuu moja la L02 na limepangiwa kutekeleza Programu kuu tatu (3) zenye Programu ndogo sita (6) ambazo kwa ujumla wake zinajumuisha shughuli na huduma zote zinazokusudiwa kutekelezwa na Wizara hii, katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatarajiwa kukusanya jumla ya Tsh Bilioni 5,727,275,000 kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Aidha, Wizara inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh Bilioni 81,061,012,000. Kati ya fedha hizo Tsh Bilioni 9,313,000,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida ambapo Tsh Bilioni 3,814,300,000 ni Mishahara, Tsh Bilioni 2,452,400,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Uendeshaji wa Ofisi na Tsh Bilioni 3,046,300,000 ni Ruzuku kutoka SMZ ambayo ni kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na Kampuni ya Uvuvi Zanzibar. Kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Wizara imetengewa Tsh 71,748,012,000 ambapo TZS 35,500,000,000 kutoka SMZ na TZS 36,248,012,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza Wizara kwa kuanzisha miradi mipya na kuendeleza miradi mengine ambayo ilianza tokea mwaka wa bajeti unaoishia tarehe 30, June 2022/2023, Miradi hiyo mipya na ambayo inaendelea kwa ujumla wake itakua ni kumi na sita (16) ambapo baadhi ya miradi hiyo inatarajiwa kukamilika hivi karibuni, ukamilikaji wa miradi hiyo itaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa visiwa vya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ridhaa yako sasa naomba nitoe maoni ya Kamati ya Uchumi kwa Programu Kuu za Wizara hii ambazo Kamati yangu imezitolea maelekezo na ushauri kama ifuatavyo:

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu hii ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu imeundwa na Programu ndogo moja ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu na Huduma sita (6) ambazo zinatekelezwa na Idara ya Maendeleo na Uratibu wa Uchumi wa Buluu (Pamoja na Mafuta na Gesi). Aidha, lengo kuu la Programu Kuu hii ni Kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu. Programu hii kwa mwaka wa Fedha 2023/2024, imeombewa jumla ya Tsh Bilioni 17,147,383,000. Fedha hizo ni ongezeko la Tsh. Bilioni 2,943,582,000 kutoka kwenye bajeti ya mwaka unaoishia June 30, 2023 ambayo ilikuwa ni 14,203,801,000.

Kamati yangu ilitaka kujua sababu hasa zilizopelekea ongezeko hilo kubwa la kifedha na kuarifiwa kuwa huduma ya HL02010106 ya Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Bahari (Bahari Maisha) ndio iliokuza engezeko hilo kwa kupatiwa kiasi cha Tsh.Bilioni sita (6) ambazo kwa bajeti inayoishia June 2023 hakukuwa na huduma hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ndiyo inayoshughulikia masuala yote ya udhibiti, ufuatiliaji, na uendelezaji wa shughuli za Mafuta na Gesi Nchini. Kamati yangu haijaridhishwa na hatua zinazochukuliwa kwenye vipengele vilivyo chini ya program hii, kwa kampuni ya utafutaji wa mafuta (ZPDC), toka ilivyoanzishwa kampuni hii imeshindwa kujiendesha yenyewe, na hadi sasa kampuni hiyo inapokea ruzuku ya fedha za mishahara Pamoja na fedha za uendeshaji wa kampuni hiyo kutoka Serikalini jambo ambalo halikua lengo la kuanzishwa kwa kampuni hiyo.

Aidha, Kamati yangu imesikitishwa na ucheleweshaji wa kupatiwa hati miliki ya eneo litakalojengwa bohari ya kuhifadhia mafuta kwa ajili ya kampuni ya ZPDC kwani Kamati inatambua kuwa ZPDC ni kampuni ya Serikali na Taasisi inayohusika na utoaji wa hati miliki ya ardhi hiyo ni ya Serikali hivyo ni lazima wakae kwa pamoja ili kulitafutia ufumbuzi suala hilo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imeshtushwa na kuchelewa kwa uanzishwaji wa kituo cha kuhifadhia taarifa za mafuta na gesi Asilia (national data respository NDR) ambayo ipo chini ya huduma ya HLO2010105. Ikumbukwe kuwa, huduma hii ilitengewa jumla ya kiasi cha Tsh Bilioni 5,000,000,000 kwa bajeti inayoishia june 30, 2023 ambapo kituo hicho hakikuweza kujengwa kutokana na kutopatiwa fedha za ujenzi, lakini kwa bajeti ijayo ya 2023/2024 huduma hiyo inaombewa kiasi kidogo zaidi cha Tsh bilioni 4,000,000,000. Jee, ni kiasi gani cha fedha hizo zitakazopatikana?

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaitaka Serikali kuipa kipaumbele huduma ya ujengwaji wa kituo hicho, ili kuhakikisha taarifa za upatikanaji wa mafuta na gesi zinapatikana kwa uhakika na kwa usahihi, kwani kituo hicho ndicho kitakachotumika kwenye kuuza data kwa kampuni zitakazohitaji taarifa sahihi zilizopatikana kwenye hatua mbalimbali wakati wa utafiti wa utafutaji wa mafuta. Ikumbukwe kuwa, tafiti hizo zilitumia fedha nyingi wakati wa kukusanya taarifa hizo na endapo taarifa hizo zikishindwa kuhifadhiwa vizuri huenda zikapotea, hali ambayo itaisababishia Serikali kuingia hasara tena kwenye suala la utafiti kwa maeneo ambayo tayari yalishafanyiwa utafiti huo hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaitaka Serikali, kulimaliza suala la kuwalipa fidia wananchi waliothirika na mtetemo wakati wa zoezi la utafiti na utafutaji wa mafuta kwani kadri muda unavyozidi kusonga mbele na thamani ya fedha wanazodai inazidi kupungua. Sambamba na hayo, Kamati yangu inasisitiza kwa mara nyengine tena suala la kuendelea na utafiti wa utafutaji wa mafuta na gesi liwe endelevu. Aidha, Naiomba Wizara iendelee kufanya Tafiti za kina katika masuala mazima ya Mafuta na Gesi, kwani wananchi wengi wamekua na hamu ya kutaka kujua ni lini hasa rasilimali ya mafuta na gesi itaanza kutoa matunda kwa uchumi wetu.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi imeundwa na Programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini na Programu ndogo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari. Programu zote hizi kwa pamoja zinatekelezwa na Idara ya Uvuvi na Maendeleo ya Mazao ya Baharini pamoja na Idara ya Uhifadhi wa Bahari. Aidha, Programu Kuu hii ina lengo la kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini kwa njia ya ufugaji. Kupitia program ndogo mbili na huduma kumi na nne,

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya 57,513,842,000 katika kutekeleza shughuli mbalimbali za programu hii. Kamati yangu ilihoji sababu kuu iliopelekea upungufu mkubwa wa kifedha kutoka Tsh Bilioni 73,161,643,000 kwa bajeti inayoishia June 2023 hadi kiasi cha 57,513,842,000 kwenye Program hii kwa 2023/2024. Kamati yangu ilijibiwa ya kwamba sababu iliopelekea upungufu huo ni kupunguzwa kwa matumizi ya OC kwenye Program hiyo na nyenginezo. Kamati yangu inaiomba Wizara kwa kiasi hichohicho kidogo kilichotengwa, kukitumia kama kilivyopangwa kutekeleza kwa ufanisi shughuli za kimaendeleo kwa ajili ya kuinua pato la wavuvi.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunatoa pongezi za dhati kwa Wizara kwa kutoa mafunzo kwa wafugaji wa mazao ya baharini kila mwaka ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imejipangia kutoa elimu ya uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini Unguja na Pemba kwa vikundi vipatavyo 350. Tunaiomba Wizara kuendelea kutoa mafunzo kwa vikundi hivi na kuvifikia vikundi vyengine vinavyojishughulisha na uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini ili kuleta tija na kuongeza kipato kwa wavuvi. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuchukua juhudi za ziada za kuwasaidia kwenye kutataua changamoto zinazowakabili wafugaji wa samaki hasa kwenye eneo la kuvua vifaranga vya samaki kwani wafugaji hao wamekuwa wakipoteza vifaranga vingi wakati wa kuvitoa

baharini na kuvifikisha kwenye mabwawa.

Ingawa mafunzo hayo yamefanyika, Kamati yangu imebaini mapungufu kwenye zoezi la utengenezaji na ugavi wa boti za uvuvi. Jumla ya boti 577 zilitakiwa kutengenezwa kutoka katika kampuni mbalimbali za Bara na Visiwani, ambapo hadi sasa Wizara imefanikiwa kupokea asilimia 29% tu ya boti hizo ingawa muda wa kuziwasilisha boti hizo tayari umeshapita.

**Mheshimiwa Spika,**

Hifadhi ya bahari ni suala muhimu katika kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za baharini kwa vizazi vijavyo. Kamati yangu inatoa pongezi za dhati kwa Serikali kwa kazi kubwa ya uhifadhi wa bahari inayoifanya kupitia wadau mbali mbali wakiwemo Wizara hii ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Kikosi Maalum cha Kuzuwia Magendo (KMKM). Hata hivyo, kumejitokeza malalamiko ya baadhi ya wavuvi kutokutendewa haki na walinzi wa maeneo ya hifadhi wanapokuwa kwenye shughuli zao za kila siku. Hivyo, Kamati yangu inaiomba Serikali kuwashughulikia wavuvi hao kwa mujibu wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza Serikali ya awamu ya nane (8) inayongozwa na Dkt Hussein Mwinyi kwa kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa ukamilishaji wa Diko na Soko la kisasa la kuuzia Samaki la Malindi ambalo limekwenda kutatua kero ya muda mrefu iliokua ikiwakabili wavuvi, wachuuzi na hata wanunuzi wa Samaki. Hatuna budi kumpongeza tena Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwani amekua akiitekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020/2025 kwa vitendo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imearifiwa ya kwamba, mamlaka ya kiutawala ya Diko la Malindi yamehamishwa kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na kupelekwa kwa Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Kimsingi, Kamati inaunga mkono uamuzi huo, kwani Afisi ya Rais Tawala za

Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ ndio inayohusika na mambo yote ya kijamii inayohusu wananchi moja kwa moja. Aidha, Kamati yangu inaishauri Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kushirikiana na Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ kwenye kusimamia usafi wa soko hilo, kwani itakua sio busara kwa soko lililojengwa kwa fedha nyingi za Serikali ya Zanzibar na za mfadhili kutoka Serikali ya Japan kuwa katika hali ya uchafu kama lilivyokuwa awali kabla ya matengenezo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza Wizara kwa kukamilisha zoezi la ununuzi wa boti zilizotokana na fedha za ahueni ya UVIKO 19. Sambamba na hilo Kamati yangu inaitaka Wizara kukamilisha zoezi la ugawaji wa boti hizo kwa ajili ya wakulima wa mwani na wavuvi wadogo wadogo pamoja na zana zake zinazohusika ikiwemo mashine na vifaa vya kutafutia Samaki ili waweze kujikwamua na umasikini. Aidha Kamati yangu inaitaka Wizara kuwafuatilia wanavikundi waliopewa boti hizo kwani baadhi yao wamekua wakibadilisha matumizi ya boti hizo na kulifanya lile lengo la Serikali kushindwa kufikiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia fedha hizo za UVIKO 19, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imewafikia wafugaji wa mazao ya baharini kwa kuwapatia mabwawa ya ufugaji wa mazao hayo. Katika ziara yake, Kamati yangu iliyatembelea baadhi ya mabwawa hayo Unguja na Pemba na kubaini kuwa wajasiriamali hao wamejenga matumaini na mradi huo na kuwekeza nguvu nyingi lakini wanakosa nyenzo muhimu ya kufanyia kazi yao ambayo ni chakula cha kulisha samaki hao. Ingawa Kamati yangu iliarifiwa kuwa Wizara imeagiza mashine ya kutengeneza chakula hicho kwa jumla ya shilingi za kitanzania milioni 139.5 kwa kampuni binafsi, kwa masikitiko makubwa mashine hiyo haijawasilishwa nchini hadi leo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaiomba Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Programu ndogo ya maendeleo ya Uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini kuendelea na utafiti wa mwani mnene (Cottonii) katika maeneo tofauti ya visiwa vyetu, kwani majaribio

yaliofanywa kwa mwani huo katika eneo la Mwambale umeonekanwa kustawi vizuri sana na pia soko la mwani huo ni zuri sana huko kwenye soko la kimataifa.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Programu ndogo Tatu, zinazojumuisha Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, Programu ndogo ya Mipango, Sera na Tafiti na Programu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Uchumi wa Buluu Afisi Kuu Pemba. Aidha, Programu Kuu hii inatekelezwa na Idara ya Utawala na Uendeshaji na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Lengo la programu hii ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi na ustawi kwa sekta. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 6,399,787,000.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuitanabahisha Wizara kwamba fedha ambazo Baraza lako Tukufu itaziidhinisha kwa Wizara hii ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni fedha za walipa kodi zinazotozwa kutoka kwa Wananchi. Hivyo, Kamati yangu inaitaka Wizara kuwa makini katika matumizi itakayoyafanya ili yale malengo waliyoyapanga yaweze kutekelezwa na Wananchi nao wanufaike ipasavyo kwa mrejesho utakaofanywa kwa matumizi mazuri ya fedha zao.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara hii kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano waliotupatia wakati wa kuipitia Bajeti yao. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati yangu imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kuipitia, kuijadili, kutoa mapendekezo yao na hatimae kuiunga mkono na kuipitisha Bajeti hii ili tumuwezeshe Mheshimiwa Waziri kutekeleza yale aliyojipangia katika mwaka ujao wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kusema hayo, Kwa niaba ya Kamati yangu ya Uchumi naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,



……………………………

Mhe. Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Uchumi,

Baraza la Wawakilishi,

**<u>Zanzibar.</u>**